# MABADILIKO KATIKA SHERIA YA MANUNUZI YA UMMA YA MWAKA 2023 NA KANUNI YA MWAKA 2024



*Cpsp Werema M Chacha, Supplies Office , Kondoa Town Council*

## Utangulizi

Ununuzi wa Umma ni shughuli muhimu ya kiuchumi inayohusisha sehemu kubwa ya Pato la Taifa (GDP). Takribani asilimia 70 ya Bajeti ya Serikali na Taasisi zake hutumika kwenye ununuzi wa umma. Ununuzi wa Umma nchini unasimamiwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410

**Dondoo**

i. *Historia ya Sheria ya Ununuzi wa Umma (Sura 410) na Mabadiliko na Mabadiliko yake*

ii. *Mafanikio katika Ununuzi wa umma*

iii. *Sababu za Mapendekezo ya Kutungwa Upya Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2023*

iv. *Mabadiliko Muhimu katika Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma*

**Historia ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na Mabadiliko yake.**

✓ Kabla ya mwaka 2001, shughuli za ununuzi na ugavi Serikalini ziliongozwa na Financial Orders Part III, 5thEdition, 1965, Serikali iliendelea kutumia Financial Orders Part III hadi Mwaka 2001

✓ Mwaka 2001 Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.3 ya Mwaka 2001 ilitungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kufuta Financial Orders Part III, 5th Edition, ya mwaka 1965.

✓ Kutokana na upungufu uliokuwepo katika Sheria Na. 3 ya Mwaka 2001, Serikali iliifuta sheria hiyo na kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004.

***Baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004 ni pamoja na:***

✓Kuiondoa Central Tender Board;

✓Kuzipa mamlaka taasisi nunuzi kufanya maamuzi yote ya ununuzi kupitia Bodi za Zabuni za Taasisi Nunuzi (Tender Board)

✓Kuanzishwa kwa Vitengo vya Usimamizi wa Ununuzi (PMU)

✓Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA)

✓Kuanzisha Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma (PPAA)

**Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 07 ya Mwaka2011:**

✓ Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004 ilifutwa na kutungwa kwa Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011.

▪ ***Baadhi ya mambo yaliyozingatiwa katika kutunga sheria hii:***

✓Kuingizwa kwenye Sheria Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma (PPD)

✓Kuanzishwa utaratibu wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki;

✓Kuweka utaratibu wa ununuzi wa baadhi ya vifaa vilivyotumika;

***ii. Mafanikio mbalimbali yameweza kupatikana kupitia mabadiliko ya Sheria kati ya mwaka 2001 hadi 2023. Baadhi yake ni haya yafuatayo:***

✓Kuendelea kuongezeka kwa kiwango cha ukidhi wa Sheria

✓Ununuzi wa Umma kufanyika kwa njia ya Kielektroniki

✓Kuandaliwa na kuanza kutumika kwa Kanuni za Maadili kwa Watumishi wa Umma na Wazabuni wanaoshiriki katika shughuli za ununuzi wa umma

✓Ununuzi wa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji, wasambazaji na mawakala wakubwa; na ✓Kuongezeka kwa hadhi ya vitengo vya usimamizi wa ununuzi.

***iii: Sababu za Mapendekezo ya Kutungwa kwa Sheria Mpya ya Ununuzi mwaka ya 2023***

✓ Bei kubwa za Bidhaa, Huduma na Kandarasi ikilinganishwa na bei ya soko

✓ Kukosekana kwa viwango vya ukomo wa uidhinishaji wa zabuni

✓ Usimamizi hafifu wa masuala ya Mnyororo wa Ugavi pamoja na masuala hayo kutofungamanishwa na ununuzi katika Sheria

✓ Matumizi mabaya ya Utaratibu wa "Force Account" katika utekelezaji wa Miradi

✓ Usimamizi hafifu wa Mikataba ya Ununuzi kutokana na ukosefu wa masharti mahsusi katika Sheria yanayohusu usimamizi wa mikataba

✓ Sheria kutotofautisha masharti ya ununuzi kati ya taasisi za umma zinazojiendesha na zisizojiendesha kibiashara

✓ Sheria kutoa mwanya wa ununuzi kutekelezwa nje ya mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki, hivyo kusababisha matumizi hafifu ya Mfumo

✓ Kutokuwepo kwa sharti la bei kikomo katika ununuzi wa umma

✓ Sheria kutokuwa na masharti ya ukomo wa thamani ya miradi, uandaaji wa taarifa ya ukaguzi wa kazi zilizofanyika; udhibiti wa ubora wa kazi iliyotekelezwa; viwango vya weledi na uzoefu wa watekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa utaratibu wa "Force Account"

✓ muda mrefu katika utekelezaji wa michakato ya ununuzi

✓ Kutolewa kwa Adhabu Mara ya pili kwa kosa moja kwa wazabuni Waliofungiwa Nje ya Nchi

v. ***Mabadiliko Muhimu katika Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma, Na. 10 ya Mwaka 2023***

▪ Wizara ya Fedha ilipokea mapendekezo ya maboresho ya Sheria hiyo kutoka kwa wadau kupitia vikao mbalimbali, Kutokana na wingi wa mapendekezo ya maboresho, Serikali iliamua kutunga upya Sheria ya Ununuzi wa Umma. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga upya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 katika kikao cha nane cha Mkutano wa 12 kilichofanyika tarehe 7 Septemba, 2023. Muswada huo ulisainiwa na Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria tarehe 29 Septemba 2023 na baada kutangazwa (Publication) tarehe 6 Oktoba 2023.

▪ Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma, Na. 10 ya Mwaka 2023, imeanza kutumika tarehe 17 Juni 2024 kama iilivyotangazwa na Waziri kwenye Gazeti la Serikali, GN No. 455/2024. Baadhi ya mabadiliko hayo ni kama ifuatavyo;

**Kifungu cha 3: Tafsiri**

✓ Tafsiri za maneno kadhaa zimeongezwa zikiwemo "Ugavi" na "Taasisi zinazojiendesha kibiashara".

**Kifungu cha 5:**

❖ Kifungu kimeandikwa upya ili kujumuisha:

✓“Thamani ya Fedha” katikavununuzi wa umma

✓Kujumuisha masuala ya “uendelezaji wa viwanda vya ndani”,

✓“maendeleo endelevu” na

✓“uhifadhi wa mazingira”Taasisi nunuzi zitatakiwa kuzingatia masuala yafuatayo ili kufikia viwango vya juu vya haki kwa kuzingatia:

✓ Fursa sawa kwa wazabuni wote,

✓ Haki sawa kwa wahusika,

✓ Uendelezaji wa viwanda vya ndani, maendeleo endelevu na

✓ Umuhimu wa kupata thamani ya fedha kwa kuzingatia viwango na vigezo vilivyoainishwa

**Kifungu cha 9: Malengo ya Mamlaka**

✓ Kuhakikisha taasisi nunuzi zinatoa upendeleo kwa wazabuni wa ndani katika zabuni za bidhaa, kazi za ujenzi na huduma (kifungu kilichoongezwa);

✓ Kufuatilia uzingatiaji wa sheria wa taasisi nunuziKifungu cha 10: kufungamanisha majukumu ya PPRA na masuala ya usimamizi wa mnyororo wa ugavi (Ununuzi, Ugavi na Usambazaji).

✓ PPRA Kudhibiti ununuzi wa washauri elekezi, washauri wa miradi na mtu binafsi kuhusiana na miradi ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;

**Kifungu cha 30**: Uwasilishwaji wa Taarifa ya Mwaka ya Tathmini ya Utendaji kazi wa ununuzi wa Umma na Thamani Halisi ya Fedha kwa Rais kila ifikapo au kabla ya tarehe 30 Machi kila mwaka.

**Kifungu cha 32: Bodi ya Zabuni.**

✓ Sheria imeongeza vifungu vipya vidogo vinavyohusu mamlaka ya Bodi ya zabuni na Afisa Masuuli katika uidhinishaji wa ununuzi kwa kuzingatia ukomo wa uidhinishaji.

**Kifungu cha 49: Taasisi za Kibiashara.**

✓ Sheria imeweka kifungu kinachoweka masharti mahsusi kupitia Kanuni kuhusu utaratibu utakaozingatiwa na Taasisi za Umma zinazojiendesha kibiashara katika ununuzi wa umma.

**Jedwali la 10 na 11: Kupunguza muda wa Mchakato**.

**Kifungu cha 56-61: Upendeleo kwa bidhaa, watu na Kampuni za Ndani**.

➢ Upendeleo wa Kitaifa

➢ Upendeleo wa kipekee kwa watu au Kampuni za Ndani

➢ Ushiriki wa Kampuni za ndani na wataalamu katika mikataba ya ushauri elekezi

**Kifungu cha 62**: **Uingiaji wa Ushirika au Mikataba midogo na Kampuni za ndani**.

✓Kwa ununuzi wa kazi za ujenzi na huduma zisizo za ushauri wa kitaalamu zaidi ya ukomo uliyoainishwa katika Kanuni, Taasisi Nunuzi inapaswa kuwataka wazabuni wa kigeni kuingia ushirika au mikataba mdogo na Kampuni za ndani.

**Kifungu cha 63: Umiliki wa mtaji wa hisa**

✓Kampuni za ndani zitapaswa kuwa na mtaji wa hisa ambao wote unamilikiwa na raia wa Jamhuri ya Muungano.

**Kifungu cha 64: Upendeleo kwa makundi maalum ya kijamii**

✓Taasisi nunuzi itatenga kiwango cha asilimia 30 ya ununuzi ya mwaka kwa ajili ya makundi maalum ya kijamii kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika Kanuni za Ununuzi wa Umma.

**Kifungu cha 128: Makosa na adhabu**

✓ kimefanyiwa maboresho ambapo itakuwa kosa la jinai kwa yeyote atakayekiuka masharti yanayohusiana na upendeleo kwa bidhaa, watu na kampuni za ndani.

**Kifungu cha 72: Kufungiwa mzabuni**

✓ Sheria imeondoa masharti ya mzabuni aliyefungiwa nje ya nchi kupewa adhabu ya ziada ya kufungiwa kwa kipindi cha miaka 10 kwa makosa ya udanganyifu au rushwa, au miaka 5 kwa makosa mengine.

**Kifungu cha 73: Ununuzi kwa njia ya Kielektroniki**

✓ Katika sheria hii sharti linalotoa mwanya kwa Taasisi nunuzi kufanya ununuzi nje ya mfumo wa kielektroniki limeondolewa.

**Kifungu cha 74: Bei Kikoma**

✓ Sheria imeweka masharti kwa Taasisi nunuzi kununua bidhaa, huduma na kazi za ujenzi kwa kuzingatia bei kikomo kadiri zitakavyokuwa zimeandaliwa na mamlaka

**Kifungu cha 76: Matumizi ya rasilimali za ndani (Force Account)**

➢Sheria imeweka masharti yanayohusu matumizi ya rasilimali za ndani ***(force account)*** yakiwemo:

✓ uzingatiaji wa ***ukomo wa thamani***,

✓ hitaji la kuwa na ***wataalamu wenye weledi*** na vifaa kwa ajili ya kusimamia miradi

**Kifungu cha 82: Ununuzi wa Bidhaa za Afya**

✓ Sheria imeweka masharti ya ununuzi wa bidhaa za afya,

✓ Wizara yenye dhamana na masuala ya afya itaandaa na kuidhinisha viwango vya bidhaa za afya vitakavyotumiwa na Bohari ya Dawa kwa ununuzi wa bidhaa za afya.

**Kifungu cha 93 hadi 98: Usimamizi wa Mikataba**

➢Sheria imeongezwa sehemu mpya inayohusu masuala ya Usimamizi wa Mikataba.

✓ Lengo ni kuweka masharti yanayohusu usimamizi wa mikataba ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa, kazi za ujenzi na huduma zenye ubora kulingana ***value for money***

**Kifungu cha 93 - kusimamia utekelezaji wa mkataba**

✓ Katika sheria hii, Afisa Masuuli ana wajibu wa jumla kuhusu utekelezaji wa mkataba kwa namna itakavyoainishwa katika kanuni.

✓ Idara tumizi itakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa mkataba kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

✓ Idara tumizi itapendekeza kwa Afisa Masuuli kuteua kwa kila mkataba, msimamizi wa mkataba ambaye atakuwa na wajibu wa kuhakikisha utekelezaji wa mkataba uliyosainiwa.

**Kifungu cha 94 - Udhibiti wa gharama, ubora na muda mikataba**

➢ Katika sheria hii, Idara tumizi itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zilizotolewa:

✓zimekidhi vigezo na masharti ya mkataba;

✓zimezingatiaa ubora na gharama ili kuhakikisha ***Value for Money.***

**Kifungu cha 96 - Malipo ya awali**

✓ Katika sheria hii, kazi za ujenzi, bidhaa au huduma hazitalipiwa kabla hazijatekelezwa, kuwasilishwa au kutolewa na kukubaliwa na afisa masuuli au afisa aliyeidhinishwa na afisa masuuli.

✓ Malipo ya awali hayatalipwa kabla mkataba haujasainiwa na yatakuwa katika kiwango kitakachoainishwa katika kanuni au mwongozo

**Kifungu cha 100 - Wajibu wa taasisi nunuzi katika usimamizi wa bidhaa, au mali**

✓ Taasisi nunuzi imepewa wajibu wa kusimamia bidhaa, vifaa au mali zilizopokelewa kwa lengo la kuzuia upotevu na uharibifu na kuendeleza matumizi.Mabadiliko Muhimu katika Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma

✓ Ili kuepuka kushikilia fedha pasipo na faida, taasisi nunuzi itahakikisha bidhaa na vifaa vinatunzwa kwa idadi ndogo yenye ulazima kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za taasisi kwa ufanisi.

✓ Tasisi nunuzi itaweka mifumo ya kielektroniki ya kudhibiti na kusimamia bidhaa, vifaa au mali kwa madhumuni ya kufikia malengo thabiti ya usimamizi wa mnyororo wa ugavi

**Kifungu cha 99-104 - Usimamizi wa Ugavi**

✓ Sheria imeweka sehemu ya nane kwa ajili ya usimamizi wa ugavi na mali.

✓ Sehemu hii inaenda sambamba na maboresho ya Kitengo cha Ununuzi ambacho kilikuwa na Maafisa Ugavi ambao walisimamiwa na Sheria ya Fedha

## Kanuni za Ununuzi Wa Umma mwaka 2024

**Kanuni ya 4: Uhifadhi wa mazingira**

• Kuhakikisha utekelezaji wa mikataba unazingatia wajibu uliobainishwa katika masharti ya uhifadhi wa mazingira na kutunza kumbukumbu ya utekelezaji huo; na

• matumizi na uondoshaji wa bidhaa, vifaa au mali unafanyika kwa kuzingatia misingi ya uhifadhi wa mazingira.

▪ **Kanuni ya 11: Mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa Umma**

Kwa kuzingatia kifungu cha 73 cha Sheria, taasisi nunuzi zitapaswa kufanya shughuli za ununuzi, ugavi na uondoshaji mali zilizoainishwa katika Kanuni hizi kupitia mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma.

**Kanuni ya 88 na 309. Usimamizi wa Mikataba ya Ununuzi**

✓ Afisa masuuli atawajibika katika utekelezaji na usimamizi wa mikataba ya bidhaa, huduma au kazi za ujenzi ambazo zinazotekelezwa na taasisi nunuzi na atapaswa

▪ **Kanuni ya 23: Dhamana ya Zabuni**

Dhamana ya zabuni au tamko la dhamana ya zabuni litaendelea kuwa halali kwa muda usiopungua siku ishirini na nane zaidi ya muda wa uhai wa zabuni, ili kuipa taasisi nunuzi muda wa kuchukua hatua kama dhamana itaitishwa ***(Kan.24)***

▪ **Kanuni ya 29: Dhamana ya utekelezaji wa mkataba**

✓ Pale ambapo mazingira yanalazimu marekebisho ya mkataba baada ya kusainiwa, na marekebisho hayo kutekelezwa, taasisi nunuzi itamtaka mzabuni au mshauri elekezi mshindi kuwasilisha dhamana ya ziada ya utekelezaji wa mkataba ili kutosheleza ongezeko lolote la jumla la zaidi ya asilimia kumi ya bei ya mkataba

▪ **Kanuni ya 31: Bei Kikomo**

✓ Bei kikomo itakayopatikana itawekwa kwenye mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma na inaweza kutumika kulingana na kanda, mikoa na wilaya kadiri itavyoamuliwa na Mamlaka

**Kanuni ya 32: Kukuza viwanda vya ndani**

✓ Taasisi nunuzi zitahakikisha ununuzi unaofanyika unalenga kukuza viwanda vya ndani na kusaidia maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia-

(a) masharti ya vigezo vya kufaidika na mpango wa upendeleo na hifadhi;

(b) ukomo wa asilimia ya upendeleo, endapo utatumika

(c) aina ya bidhaa, kazi za ujenzi na huduma zilizotengwa au kuhifadhiwa kwa ajili ya makundi maalumu

(d) njia za kupima ufanisi wake katika kufikia malengo

**Kanuni ya 35: Upendeleo wa kipekee kwa makundi maalumu**

✓ Taasisi nunuzi itatoa upendeleo wa kipekee wa asilimia thelathini katika ununuzi wake wa mwaka wa bidhaa, kazi za ujenzi na huduma kwa makundi maalumu yaliyopo katika eneo lake

✓ Taasisi nunuzi itatoa sababu ya kushindwa kukidhi matakwa ya upendeleo wa kipekee

**Kanuni ya 37: Vigezo vya upendeleo kwa wazawa na kampuni za ndani**

✓ Mtu au kampuni itastahili kunufaika na mipango ya upendeleo ikiwa mtu au kampuni hiyo inakidhi sifa zilizoainishwa katika kifungu cha 56(4) cha Sheria

**Kanuni ya 39: Uingiaji wa ushirika**

✓ Wazabuni wanaweza, kwa lengo la kupata upendeleo katika zabuni za ununuzi wa umma, kuingia katika ushirika

✓ Ushirika utakaoingiwa unaweza kuwa ni ushirika kati ya kampuni za ndani pekee au kati ya kampuni ya ndani na kampuni ya kigeni

**Kanuni ya 40: Uingiaji wa mkataba mdogo**

✓ Mkataba wowote wa ushirika utakaoingiwa kati ya kampuni ya kigeni na kampuni ya ndani utakuwa ni sehemu ya mkataba wa ununuzi utakaoingiwa.

✓ Kampuni ya kigeni iliyopewa tuzo ya mkataba wa ununuzi inaweza, kwa lengo la kupata upendeleo katika zabuni za ununuzi wa umma, kuingia kwenye mkataba mdogo na kampuni ya ndani.

✓ Taasisi nunuzi itatoa ukomo wa upendeleo hadi asilimia sita kwa kampuni ya kigeni ambayo itatoa mkataba mdogo kwa kampuni ya ndani kama ulivyoainishwa katika **Jedwali la Nane la kanuni**

**Kanuni ya 41: Uingiaji wa Ubia**

- Wazabuni wanaweza, kwa lengo la kupata upendeleo katika zabuni za ununuzi wa umma, kuingia katika ubia.
- Ubia utakaoingiwa unaweza kuwa ni ubia kati ya wazabuni wa ndani pekee au kati ya wazabuni wa ndani na wazabuni wa kigeni Mambo Muhimu yaliyowekwa katika Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024
- Mzabuni wa ndani atakayeingia katika ubia na mzabuni wa kigeni atakuwa na ubia usiopungua **asilimia hamsini na moja (51%)** ya mtaji wa hisa zilizolipwa katika ubia na isiyopungua **asilimia hamsini (50%)** kwa kutoa wataalamu wanaotakiwa zkatika kutekeleza mkataba

**Kanuni ya 49. Mafunzo kwa vitendo**

✓ Katika utekelezaji wa kazi za ujenzi na huduma za ushauri elekezi wakandarasi na washauri elekezi watapaswa kutoa nafasi ya kujifunza kwa vitendo kwa wataalamu wahitimu kwa ajili ya kujenga uwezo.

✓ Wataalamu wahitimu watachukuliwa kutoka katika mpango wowote wa mafunzo kwa vitendo unaotambulika au kusimamiwa na Serikali

**Kanuni ya 50. Malipo kwa Wakati**

✓ Taasisi nunuzi kuhakikisha kwamba malipo yanafanyika kwa wakati kwa wazabuni kwa lengo la kusaidia ukuaji wa kampuni za ndani na kuziwezesha kampuni hizo kutimiza wajibu wao wa kimkataba.

✓ Taasisi nunuzi itapaswa, kabla ya kusaini mkataba chini ya mpango wa upendeleo uliotengwa, kuhakikisha kuwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mkataba zimetengwa na kuidhinishwa.

**Kanuni ya 55. Ununuzi katika ngazi za chini za serikali za mitaa**

✓ Kwa kuzingatia kanuni za 52, 53 na 54, afisa masuuli anaweza kukasimisha mamlaka ya ununuzi kwa wasimamizi wa ngazi za chini za serikali za mitaa kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa shughuli za ununuzi

✓ Ununuzi katika ngazi za chini za serikali za mitaa utafanyika kwa kuzingatia mwongozo utakaotolewa na Mamlaka

**Kanuni ya 74. Ununuzi wa dharura**

✓ Baada ya kukidhi masharti hayo afisa masuuli ataendelea kufanya ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma kwa mujibu wa njia ya ununuzi iliyochaguliwa na kwa mujibu wa kifungu cha 77(4) cha Sheria.

✓ Afisa masuuli atawasilisha maombi ya idhini ya kuhalalisha ununuzi uliokwishafanyika kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kutoa mkataba na kueleza mazingira ambayo yalimzuia kufuata utaratibu wa kawaida wa ununuzi

**Kanuni ya 77. Uwajibikaji wa afisa masuuli**

✓ Endapo ununuzi umefanyika usio wa muhimu au wenye ubadhilifu; au kushindwa kufanya tathmini au kuchukua hatua kwa wakati –

❖ Afisa masuuli atawajibika kwa hatua za kinidhamu na

❖Atapaswa, pamoja na adhabu yoyote atakayopewa, kulipa tofauti kati ya gharama halisi ya ununuzi na gharama ambayo ingetumika kama angetumia njia sahihi.

**Kanuni ya 79. Mpango wa Ununuzi**

✓ Taasisi nunuzi wakati wa uandaaji wa mpango wa ununuzi itaandaa makadirio yake kulingana na bei kikomo iliyoainishwa chini ya Kanuni; au kwa kutumia bei za soko, endapo hakuna bei kikomo iliyoainishwa

✓ Katika kujumuisha mipango hiyo, taasisi nunuzi itaweka njia sahihi ya ununuzi itakayotumika kwa kila hitaji.

**Kanuni ya 108. Uwasilishaji wa malalamiko au migogoro kwa afisa masuuli na Ushughulikiaji wake**

✓ Afisa masuuli atashughulikia malalamiko au migogoro iliyowasilishwa na wazabuni kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma.

**Kanuni ya 133. Ununuzi wa bidhaa za afya**

✓ Vituo vya kutolea huduma ya afya bila kujali uanzishwaji wake wa kisheriavitatakiwa kununua bidhaa za afya za aina zote kutoka kwa Bohari ya Dawa.

✓ Kanuni 135 imeweka utaratibu wa uharakishaji wa ununuzi wa bidhaa za afya ikiwa ni pamoja na kupunguza muda, na kuwasilisha mkataba kwa Mwanasheria Mkuuikiwa na **notisi ya dharura**

## Hitimisho